


BARAZA LA TAIFA LA ELIMU YA UFUNDI



SIFA ZA UDAHILI WA WANAFUNZI KWENYE KOZI MBALIMBALI

Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE) ni chombo kilichoanzishwa kwa Sheria ya Bunge Sura ya 129, ili kusimamia na kuratibu utoaji wa mafunzo ya elimu ya ufundi katika Vyuo Visivyokuwa Vyuo Vikuu au Vyuo Vikuu Vishiriki vinavyotoa mafunzo kwa ngazi za Astashahada, Stashahada na Shahada nchini. Jukumu mojawapo la Baraza, ni kuhakikisha kuwa mafunzo yanayotolewa katika Vyuo vya Elimu ya Ufundi yanakidhi viwango, vigezo na ubora unaohitajika katika soko la ajira ndani na nje ya nchi.

Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE) linapenda kufahamisha umma kuwa lina kanuni na taratibu za kuandaa mitaala inayotumika katika kutoa Elimu na Mafunzo ya Ufundi nchini. Taratibu hizo zinataka ushirikishwaji wa wadau mbalimbali katika maandalizi ya mtaala. Taasisi inayoandaa mtaala ni lazima iweze kupata mahitaji ya soko la ajira ambayo ndio yanayotengeneza maudhui ya mtaala husika. Miongoni mwa mambo ambayo mtaala unatakikiwa kuwa nayo ni sifa za kujiunga na kozi husika, ambazo lazima zisiwe chini ya sifa za jumla zilizowekwa na Baraza.

Baraza, linapenda ifahamike kwamba sifa za kujiunga na kozi husika zinapatikana kwenye mtaala wa kozi husika. Ni sifa hizo zilizopo kwenye mtaala ndizo ambazo huwa zinawekwa kwenye kitabu cha mwongozo wa udahili (Admission Guidebook) ambacho hupatika kwenye tovuti ya NACTE.

Mitaala ya kozi zote za Afya huaandaliwa chini ya uratibu wa Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. Wakati wa maandalizi ya mitaala hiyo miongoni mwa wadau wanaohusishwa ni pamoja na Bodi za Kitaaluma kama vile Baraza la Famasia, Baraza la Uuguzi na Ukunga, Baraza la Maabara na mengineyo kulinga na aina ya kozi husika. Uhusishwaji huu, unalenga kuhakikisha kwamba viwango vinavyokubalika katika taaluma husika vinazingatiwa katika utoaji wa mafunzo.

Baada ya Mtaala kuandaliwa kwa njia shirikishi ya wadau mbalimbali wa sekta husika, mtaala huwasilishwa NACTE kwa ajili ya kupitiwa ambapo Kamati ya Wataalam wenye taaluma husika hukaa na kuujadili, kisha kuwasilisha mapendekezo yake kwenye Bodi ya Masomo husika ili kuona kama unakidhi mahitaji ya soko la ajira, na baadae Mtaala huo huwasilishwa kwenye Baraza kujadiliwa na kutoa idhini ya kutumika, au la.

Hivyo, sio kweli kama inavyodaiwa na baadhi ya watu wanaoeneza taarifa za kulichafua Baraza kwamba NACTE imeamua kudahili vihiyo kwenye mafunzo ya kozi za afya kwa kuweka vigezo vya kuwachukua wanafunzi waliofeli mitihani ya kidato cha nne. Huu ni uongo wenye lengo la kupotosha umma. Hivyo watu hao wapuuzwe.

Baraza linaisitiza kwamba wale wanaoomba udahili katika kozi mbalimbali za Astashahada na Stashahada kwenye vyuo au taasisi mbalimbali wazingatie vigezo vilivyoanishwa kwenye Kitabu cha Mwongozo wa Udahili. Hivyo kama kuna taasisi yeyote inayodahili kwa kuzingatia vigezo/sifa tofauti na zilizoainishwa kwenye kitabu hicho, basi Waombaji wajue watakuwa wanatapeliwa na hivyo wawasiliane na Baraza kwa hatua za haraka.

**IMETOLEWA NA
OFISI YA KATIBU MTENDAJI
BARAZA LA TAIFA LA ELIMU YA UFUNDI (NACTE)
03/8/2018**